#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo No. 13

Januari - Machi 2024





## Dkt. Samia Amteua Dkt. Kiwia Mkurugenzi Mtendaji HESLB

Jumatano,
Februari 7, 2024

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan amemteua Dkt. Bill Kiwia kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Dkt. Kiwia anachukua nafasi ya Abdul-Razaq Badru ambaye ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Jumanne, Februari 6, 2024 na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu uteuzi wa Dkt. Kiwia unaanza Februari 6, 2024.

Dkt. Kiwia ana Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Uhasibu na Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza; Shahada ya Umahiri (MSc) kutoka Chuo Kikuu cha Strathclyde, Uingereza na Stashahada ya Juu katika Uendeshaji wa Benki kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), Tanzania.

Pamoja na uzoefu mkubwa katika kufundisha, Dkt. Kiwia ni mtaalamu wa fedha na benki akiwa amefanya kazi kwenye taasisi za fedha zikiwemo Benki za Exim, Stanbic na Benki Kuu ya Tanzania (BOT).

## NDANI...




03

**HESLB, ZEEA**
wakubaliana kimkakati



04

**VUMILIA:**
Naipongeza serikali kwa kutoa mikopo ya Stashahada



## JAMBO LETU

**Jacqueline Msuya**
*Mhariri*

## Urejeshaji wa mikopo kwa kushirikiana na wadau wa kimkakati

Nakukaribisha katika toleo hili la 13 la Jarida la mtandaoni HESLB Yako ili kwa mara nyingine uweze kujua masuala ambayo HESLB imeyapa uzito mkubwa katika robo ya mwaka iliyoanzia Januari hadi Machi 2024.

Mengi yametokea na mengine yanatarajiwa hivi karibuni kwa lengo la HESLB kuendelea kuwa moja ya taasisi zenye ufanisi mkubwa nchini hususan katika eneo la ugharimiaji wa wanafunzi katika ngazi ya vyuo vya kati na vya elimu ya juu na hivyo kuwa na uhakika wa kupata wataalamu wa sekta mbalimbali.

Itakumbukwa kuwa moja ya tukio la kukumbukwa lilitokea mwanzoni mwa mwezi Februari mwaka huu, ambapo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Dkt. Bill Kiwia kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB akichukua nafasi ya Abdul-Razaq Badru aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Tunawapongeza viongozi hawa wote wawili kwa kupokezana kijiti cha kuongoza taasisi hii inayotegemewa na watanzania katika kugharimia wanafunzi wahitaji ili waweze kufikia ndoto zao za kupata elimu ya kati na juu katika vyuo vinavyotambulika na mamlaka za ithibati ya elimu katika ngazi hizo mbili.

Baada ya pongezi hizo, turudi kwenye jambo letu, toleo hili limejikita katika kuongeza nguvu na ushirikiano wa kimkakati ili kuwafikia walionufaika na mikopo ya elimu ya juu waweze kurejesha mikopo hiyo ili iwanufaishe watanzania wengine wahitaji.

Tangu kuanza kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024 HESLB imefanya mazungumzo na kufikia makubaliano kwa kusaini hati za makubaliano (MoU) na kufungamanisha mifumo ya TEHAMA ili kuwezesha kuwabaini kwa urahisi wanufaika hususan walio katika Sekta zisizo rasmi. Baadhi ya wadau hao ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Baraza la Madaktari (MCT) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (TNMC). Taasisi hizi wadau zina kanzidata ya kutosha ya wanachama ambao wengi wao ni wanufaika wa mikopo ya elimu.

HESLB inawapongeza wadau hao na wengine walio katika hatua za mwisho za kuingia katika makubaliano rasmi na HESLB kwa kutambua umuhimu wa kurejesha mikopo ya elimu ya juu ili kuwawezesha watanzania wahitaji ambao wakielimishwa wanaongeza nguvu kazi na ujuzi kuiwezesha Tanzania kuwa nchi yenye uchumi imara.

Kwa uwekezaji wa TZS 7.2 Trilioni ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeufanya kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu tangu mwaka 1994/1995 ambayo imewanufaisha watanzania zaidi ya 754,000 na makusanyo ya TZS 2.1 Trilioni kutoka kwa wanufaika 448,823 ambao mikopo yao imeiva, bado wanufaika kadhaa wanatakiwa kujitokeza ili kurejesha mikopo yao yenye thamani ya TZS 758 Bilioni.

Kwa muktadha huo, HESLB inatoa wito kwa wadau wengi zaidi ili kuungana katika kutafuta mbinu za kuwabaini na kuwafikia wanufaika ambao hawajaanza kurejesha madeni yao yaliyoiva.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Dkt. Bill Kiwia

**Katibu**
Omega Ngole

**Mhariri**
Jacqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi

**Designer**
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067577
+255 739 067577

**Barua pepe:**
info@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



# Urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu na malengo ya kutunisha mfuko wa mikopo ya elimu nchini

HESLB imeongeza mdau muhimu wa kimkakati kwa kuingia katika makubaliano rasmi kwa kusaini hati ya makubaliano (MoU) na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) ili pamoja na mambo mengine, taasisi hizo mbili zishirikiane kuwezesha wanufaika kutafuta fursa za ajira na kurejesha fedha za mikopo walizotumia kupata elimu ya juu.

Hafla ya utiaji saini makubaliano hayo ilifanyika Machi 18, 2024 katika ofisi za HESLB jijini Dar es salaam na kuhudhuriwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi Dihenga, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia, Mkurugenzi Mtendaji wa ZEEA Juma Burhan Mohamed na watendaji wengine kutoka HESLB na ZEEA.

"Pamoja na fursa za ajira, tunaingia mashirikiano haya ili kuongeza kasi ya urejeshaji mikopo kutoka kwa wajasiriamali walionufaika na mikopo ya elimu ya juu na pia kuashiria nia njema na kuongeza ufanisi kupitia mashirikiano ya kimkakati kama tunavyoelekezwa na viongozi wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Dkt. Hussein Mwinyi," amesema Dkt. Kiwia katika hafla hiyo.

Dkt. Kiwia alibainisha kuwa, kupitia makubaliano hayo, kwa upande mmoja HESLB itaendelea kuwawezesha vijana kupata elimu kupitia mikopo na kwa upande mwingine ZEEA itawaongezea ujuzi wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu kupitia vituo atamizi (incubation centres) ili kuwaongezea uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa katika sekta binafsi hususan katika maeneo ya Utalii na Uchumi wa Buluu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa ZEEA, Juma Burhan Mohamed alisema kuwa taasisi yake inawajengea vijana uwezo kupitia vituo atamizi vilivyopo Zanzibar ambavyo vinalenga kuwaongezea ujuzi wahitimu wa vyuo vikuu.

"Tulikutana tarehe 28 Februari mwaka huu kwa mara ya kwanza, lakini kwa vile pande zote mbili tumeonesha utayari ndiyo maana leo tumeweza kufikia hatua hii ya kusaini makubaliano yatakayowezesha ufanisi zaidi kwa taasisi zetu", alifafanua Mkurugenzi Mohamed.

ZEEA ni taasisi ya umma ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibara iliyoanzishwa mwaka 2022 ili kuwawezesha wananchi kiuchumi. Aidha, HESLB ilianzishwa mwaka 2004 ili kutoa mikopo kwa wanafunzi watanzania wahitaji na kukusanya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu iliyotolewa na Serikali tangu mwaka 1994/1995.

Serikali imewekeza TZS 7.2 Trilioni kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu tangu mwaka 1994/1995 ambayo imewanufaisha watanzania zaidi ya 754,000. Licha ya kufanikiwa kukusanya TZS 2.1 Trilioni kutoka kwa wanufaika 448,823 ambao mikopo yao imeiva, bado wanufaika kadhaa hawajajitokeza ili kurejesha mikopo yao yenye thamani ya TZS 758 Bilioni.

Makusanyo ya mikopo kutoka kwa wanufaika yanaiwezesha HESLB kuchangia wastani wa 40% kwa ajili ya kukopesha wanafunzi wa elimu ya juu na kati kila mwaka. Kutokana na umuhimu huo, HESLB inaendelea kuwakaribisha wadau wengi zaidi ili kuungana katika kutafuta mbinu za kuwafikia wanufaika ambao hawajaanza kurejesha madeni yao yaliyoiva ili mfuko wa mikopo ya elimu ya juu uwe himilivu.

> *"Pamoja na fursa za ajira, tunaingia mashirikiano haya ili kuongeza kasi ya urejeshaji mikopo kutoka kwa wajasiriamali walionufaika na mikopo ya elimu ya juu na pia kuashiria nia njema na kuongeza ufanisi kupitia mashirikiano ya kimkakati kama tunavyoelekezwa na viongozi wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Dkt. Hussein Mwinyi," amesema Dkt. Kiwia katika hafla hiyo.*




# HESLB, ZEEA WAKUBALIANA KIMKAKATI

> *Kwa makubaliano haya, tunatarajia wanufaika ambao wako katika sekta isiyo rasmi watajitokeza na kuanza kurejesha mikopo yao na hivyo kufanya ongezeko la wanafunzi wahitaji kunufaika na fedha zinazorejeshwa na pia kuufanya mfuko wa kugharimia wanafunzi kuwa himilivu*

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

HESLB imesaini makubaliano na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (Zanzibar Economic Empowerment Agency - ZEEA) ili kuendelea kutafuta fursa kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu na kuongeza kasi ya urejeshaji mikopo hususan kutoka kwa wajasiriamali ambao ni wanufaika wa mikopo ya elimu.

Makubaliano hayo yalisainiwa Machi 18, 2024, jijini Dar es salaam kati ya Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia na Mkurugenzi wa ZEEA Juma Burhan Mohamed kwa niaba ya Taasisi hizo mbili za umma na kushuhudiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi Dihenga, watumishi wa ZEEA na HESLB.

Akizungumza na Waandishi wa Habari mara tu baada ya kusaini Hati ya Makubaliano (Memorandum of Understanding – MoU), Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Kiwia alisema kuwa, makubaliano hayo yanatarajiwa kuleta tija kwa wanufaika ambao wapo katika sekta isiyo rasmi akiamini watajitokeza kwa wingi na kuanza kurejesha.

Aidha, Dkt. Kiwia aliongeza kuwa, "Kwa makubaliano haya, tunatarajia wanufaika ambao wako katika sekta isiyo rasmi watajitokeza na kuanza kurejesha mikopo yao na hivyo kufanya ongezeko la wanafunzi wahitaji kunufaika na fedha zinazorejeshwa na pia kuufanya mfuko wa kugharimia wanafunzi kuwa himilivu"

Kwa upande wake Mkurugenzi wa ZEEA Juma Burhan Mohamed alibainisha kuwa anaamini kupitia makubaliano hayo, taasisi hizo mbili zitashirikiana kuandaa mafunzo kwa vijana ambayo yataleta tija na kuongeza ujuzi 'incubation' katika sekta ya utalii pamoja na fursa za ajira katika sekta hiyo.

Pamoja na mambo mengine, hati hiyo ya makubaliano kati ya HESLB na ZEEA imetaja maeneo matatu ya mashirikiano ikiwa ni pamoja na kuendelea kutafuta fursa za ajira kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu ili kuwawezesha kurejesha, kuongeza kasi ya urejeshaji mikopo kutoka kwa wajasiriamali walionufaika na mikopo ya elimu ya juu na kuashiria nia njema baina ya pande hizo mbili ambazo zimekubaliana kuleta chachu na kuongeza ufanisi katika kazi kwa maendeleo ya taifa.

Mashirikiano baina ya HESLB na ZEEA ni mwendelezo wa makubaliano ya kimkakati yaliyosainiwa katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu yanayoihusisha HESLB na Baraza la Madaktari la Tanganyika (MCT), HESLB na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (TNMC) na HESLB na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).



# VUMILIA:

## Naipongeza Serikali kwa kutoa mikopo ya Stashahada

Na Mwandishi Wetu
Mbeya

Vumilia Elia Mwakanyenda, mwanafunzi wa stashahada ya "Biomedical Engineering" katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ameipongeza Serikali kwa kutanua wigo na kuanza kutoa mikopo katika ngazi ya stashahada.

Akiongea na "HESLB Yako", Vumilia ambaye ni mnufaika wa mikopo ya stashahada iliyoanza kutolewa rasmi na Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu katika mwaka huu wa fedha wa 2023/2024, ameishukuru Serikali kwa kumpatia fursa hiyo na kuipongeza kwa kuona umuhimu wa kuwawezesha watanzania wahitaji wanaojiendeleza kielimu katika ngazi ya stashahada

"…Nyumbani kwetu ni Kyela, mkoani Mbeya na tumezaliwa watoto sita, mimi ni mtoto wa pili kuzaliwa ambaye nimefanikiwa kufikia kiwango hiki cha kupata elimu ya stashahada. Bila kupata mkopo huu, wazazi wangu wangenisomesha kwa taabu sana kulingana na kipato chao kidogo wanachopata kupitia biashara ya vyakula na matunda wanayouza kwenye genge. Ndoto zangu ni kusoma kwa juhudi ili niweza kuwasaidia ndugu zangu hapo baadaye…" anasimulia Vumilia.

Vumilia ana ndoto za kusoma hadi kupata shahada lakini anaamini pia kwa kupitia katika ngazi hii ya stashahada ataweza kupata ujuzi utakaomuwezesha kuajiriwa au kujiajiri ili aisadie familia yake na baadaye akajiendeleza katika ngazi ya shahada.

Hata hivyo, pamoja na pongezi nyingi kwa serikali, Vumilia ameiomba serikali kufikiria kutanua wigo wa utoaji mikopo ya stashahada kwa kuruhusu kukopesha programu nyingi zaidi katika ngazi ya stashahada ili kuwafikia wanafunzi wengi katika ngazi hiyo.

Kuanzia mwaka huu wa masomo wa 2023/2024, Serikali imetenga kiasi cha TZS 48 Bilioni kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi 8,000 waliodahiliwa kusoma Stashahada (diploma) katika maeneo sita ya kipaumbele ambayo yameonekana yana uhitaji zaidi wa wataalamu. Stashahada hizo ni pamoja zilizo katika fani za Afya na Sayansi Shirikishi (Health & Allied Sciences); Elimu na Ualimu (Education and Teaching); Usafiri na Usafirishaji (Transport & Logistics); Uhandisi wa Nishati (Energy Engineering); Uchimbaji Madini na Sayansi ya Ardhi (Mining & Earth Science) na Kilimo na Mifugo (Agriculture & livestock)




**Januari 22,2024,** *Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Mikopo Zambia (Higher Education Loans and Scholarships -HELSB ( katikati mwenye tai nyekundu) katika picha ya pamoja na watumishi wa Bodi hiyo, walipotembelea ofisi za HESLB- Tazara.*




**Februari 06,2024:** *Benedicto Cosmas Mkurugenzi wa Mipango, Utafiti na TEHAMA. akitoa wasilisho kuhusu mageuzi ya TEHAMA katika mkutano wa nne wa mwaka wa Serikali Mtandao uliofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC).*




**Februari 23, 2024 - Mbabane:** *Ujumbe wa HESLB katika picha ya pamoja na watumishi wa Taasisi ya mikopo ya wanafunzi nchini Swaziland (Scholarship Loan Recovery), walipowatembelea katika ofisi zao na kubadilishana uzoefu katika masuala ya utoaji na urejeshwaji wa mikopo.*



**Februari 27, 2024 – Dar es salaam:** *Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia (kulia) akipokea zawadi kutoka kwa Meneja Mwandamizi wa Benki ya CRDB Bw. Dominick Timothy alipofika ofisi za HESLB kumpongeza Dkt. Kiwia kwa kuteuliwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan na kisha wawakilishi hao wa HESLB na Benki ya CRDB kukubaliana kuendeleza mashirikiano ya utoaji huduma kwa wanafunzi.*




**Februari 27, 2024 – Arusha:** *Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Damas Ndumbaro (aliekaa katikati mbele) katika picha ya pamoja viongozi wa Serikali, viongozi wa Maafisa Mawasiliano Serikalini (TAGCO) pamoja na baadhi ya Maafisa Mawasiliano serikalini mara baada ya kufungua rasmi kikao kazi na mkutano mkuu wa mwaka wa TAGCO katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC).*



**Machi 17, 2024 – Wete, Pemba:** *Meneja Mawasiliano HESLB, Veneranda Malima (mwenye kitambaa chekundu) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya walimu na wanafunzi mara baada ya kuwaelimisha kuhusu sifa na vigezo vya upangaji wa mikopo ya elimu ngazi ya kati na juu. Wanafunzi 390 kutoka shule 15 za wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba walikusanyika katika kituo cha Sekondari ya Miti Ulaya.*




**Februari 28, 2024 – Dar es salaam:** *Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia (kulia) akipokea zawadi kutoka kwa Mkuu wa huduma za kibenki wa Benki ya NBC, Linley Kapya alipofanya ziara katika ofisi za HESLB kujitambulisha na kumpongeza Dkt. Kiwia kwa kuteuliwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan Februari 6, mwaka huu.*




**Machi 18, 2024 – Dar es salaam:** *Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Dkt. Hamisi Dihenga (aliyekaa katikati) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dkt. Bill Kiwia (mwenye tai nyekundu) na Mkurugenzi wa ZEEA, Juma Burhan Mohamed (mwenye tai ya buluu mbele) wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa HESLB na ZEEA baada ya kusaini hati za makubaliano katika ofisi za HESLB.*




# MAAFISA MAWASILIANO SERIKALINI WAPEWA SOMO ARUSHA

Februari 27, 2024
Na Mwandishi wetu

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Damas Ndumbaro amewaagiza maafisa habari serikalini kujibu hoja zinazotolewa na wananchi dhidi ya Serikali kwa kutangaza miradi na shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita ili kuwezesha wananchi kutambua juhudi zinazofanywa katika kuleta maendeleo.

Akifungua Mkutano wa siku tatu wa Chama cha Maafisa Mawasiliano Serikalini (TAGCO) kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu Mhe. Doto Biteko Februari 27, 2024, Dkt. Ndumbaro alisema maofisa mawasiliano serikalini wana wajibu wa kutangaza shughuli zinazofanywa na serikali ili kuondoa mawazo hasi miongoni mwa wananchi.

"... moja kati ya changamoto kubwa iliyoletwa na mitandao ya kijamii kwa miaka ya hivi karibuni ni kwamba, haijui ni nani mtoa habari na nani anayepaswa kujua hii ni habari. ... hivyo tumieni changomoto hizi kwa ajili ya kujibu hoja zinazotolewa mitandaoni dhidi ya Serikali", alisisitiza Dkt. Ndumbaro.

Sambamba na hilo, Waziri Ndumbaro alitoa rai kwa waandishi wa habari wa vyombo vya Serikali na maafisa habari kuhakikisha wanafanya kazi zao kwa uzalendo, weledi, ubunifu na kujibu hoja kwa wakati mara tu zinapoandikwa mitandaoni na kuwasihi kuungana kutangaza miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali badala ya kuachia taasisi na Wizara husika pekee kutoa ufafanuzi.

Awali akimkaribisha Mhe. Waziri kufungua kikao kazi cha maafisa mawasiliano serikalini, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Selestine Kakele alisema Wizara inatekeleza kwa kasi utangazaji wa sera, kanuni na taratibu za miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali, ambapo alisisitiza kwamba kazi kubwa ya Serikali ni kuhabarisha Umma kwa kutumia Maafisa Habari wake kwa kutumia mitandao ya kijamii, redio na luninga.

Kakele alitoa rai kwa baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya ambao mikoa yao haina Maafisa Habari wafanye hima kuajiri maafisa wa kada hiyo ili kutangaza kwa kasi maendeleo yanayotekelezwa na Awamu ya Sita.

Katika maelezo ya utangulizi, Kaimu Mwenyekiti wa TAGCO, Karim Meshack aliwaeleza wanachama kwamba chama kitaendelea kufanya juhudi za dhati na kuhakikisha kinawaunganisha Maafisa Habari wa Serikali ili kuwa na jukwaa moja litakalowezesha kujadili masuala mbalimbali ya Serikali pamoja na kujifunza mbinu hususani teknolojia za upashanaji habari kimkakati.

TAGCO ni taasisi inayowaunganisha maafisa habari na mawasiliano serikalini yenye lengo la kuwaunganisha na kuwainua katika utendaji wao ambapo katika kikao kazi cha siku tatu kilichofanyika Februari 27 hadi 29, 2024, jijini Arusha, maafisa habari zaidi ya 450 walishiriki kutoka Wizara, Halmashauri za miji na majiji, mashirika na taasisi za umma wakiwemo maafisa kutoka HESLB kwa lengo la kupeana uzoefu na kujifunza mbinu mpya za kuitangaza Serikali kimkakati.

> *"... moja kati ya changamoto kubwa iliyoletwa na mitandao ya kijamii kwa miaka ya hivi karibuni ni kwamba, haijui ni nani mtoa habari na nani anayepaswa kujua hii ni habari. ... hivyo tumieni changomoto hizi kwa ajili ya kujibu hoja zinazotolewa mitandaoni dhidi ya Serikali", alisisitiza Dkt. Ndumbaro.*



# PROF. MKENDA AKUTANA NA DKT. BILL KIWIA

Dodoma,
Februari 22, 2024

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amekutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Dkt. Bill Kiwia aliyefika ofisini kwa Waziri jijini Dodoma kujitambulisha rasmi baada ya kuteuliwa Februari 6 mwaka huu.

Katika kikao hicho, kilichohudhuriwa pia na Naibu Katibu Mkuu Prof. James Mdoe na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu Prof. Peter Msoffe, Prof. Mkenda ameelekeza, pamoja na mambo mengine, HESLB kuendelea kuzingatia sheria, sera na maelekezo ya Wizara na Serikali kwa ujumla katika kutekeleza majukumu yake.

Dkt. Kiwia aliongozana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi Dihenga ambao wamemshukuru Prof. Mkenda kwa ushirikiano na miongozo anayoitoa kwa HESLB ambayo inaimarisha utendaji na kuongeza tija

# MIAKA 3 YA MAFANIKIO UGHARIMIAJI ELIMU YA JUU

## Dkt. Samia Suluhu Hassan
## Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Ongezeko la Bajeti ya Mikopo na Wanafunzi** wanufaika Bajeti ya jumla kuongezeka kutoka **TZS 570 bilioni** hadi **TZS 786 bilioni**

| Mwaka wa Fedha | Bajeti (TZS Bilioni) | Idadi ya Wanufaika mwaka wa kwanza | Idadi ya wanafunzi wanufaika wote vyuoni |
|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 570 | 72,979 | 177,892 |
| 2022/2023 | 654 | 73,323 | 198,105 |
| 2023/2024 | 731 | 78,577 | 223,206 |

Kuanzishwa fursa za **'Samia Scholarships'** kwa wanafunzi wenye ufulu wa juu Kwa mara ya kwanza, mwaka **2022/2023**, fursa za **'Samia Scholarships'** zilianzishwa kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika mitihani ya Kidato cha Sita katika tahasusi za sayansi

| Mwaka wa Fedha | Bajeti (TZS Bilioni) | Idadi ya Wanufaika |
|---|---|---|
| 2022/2023 | 3 | 636 |
| 2023/2024 | 6 | 1,276 |

### Mikopo kwa Stashahada

Kuanzia mwaka **2023/2024**, wanafunzi wa stashahada (Diploma) wameanza kupata mikopo

| Mwaka wa Fedha | Bajeti (TZS Bilioni) | Idadi ya Wanufaika Iliyotarajiwa |
|---|---|---|
| 2023/2024 | 48 | 8,000 |

### Kuongeza kiwango cha fedha za kujikimu

Kuongeza kiwango cha fedha za kujikimu kwa siku kwa wanafunzi wote wanufaika

| Mwaka wa Fedha | Kiwango cha pesa ya kujikimu kwa siku |
|---|---|
| 2022/2023 | TZS 8,500 |
| 2023/2024 | TZS 10,000 |

### Urejeshaji wa mikopo

Kuondolewa kwa Tozo na Adhabu ili kuwawezesha wanufaika kurejesha Katika kipindi cha miaka mitatu **[Machi 2021 – Machi 2024]** zimekusanywa **TZS 465 bilioni**



HESLB Tanzania HESLB Tanzania HESLB_Tanzania

#KaziIendelee
#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu


## DODOMA

Jengo la PSSSF,
Br. Makole,
eneo la Uhindini

S.L.P 984,
Dodoma

+255 758 067577

+255 739 067577

info@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA

PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini
Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068,
Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Email: info@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
1 Mtaa wa Kilimo, Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068, 15471
Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Email: info@heslb.go.tz

## ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900, Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Email: zanzibar@heslb.go.tz

## ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712, Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Email: arusha@heslb.go.tz

## MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa ya pili
Br. Kenyatta
S.L.P 3051, mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Email: mwanza@heslb.go.tz

## MBEYA

Jengo la CAG, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Email: mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya pili
S.L.P 969, Mtwara
Simu: 0733 068 171
Email: mtwara@heslb.go.tz